JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# MWONGOZO WA TUZO YA RAIS YA KUHIFADHI MAZINGIRA



# DIBAJI

Nchi yetu inakabiliwa na changamoto za uharibifu wa mazingira kama vile uharibifu wa ardhi, kupotea kwa bioanuai na makazi ya wanyamapori, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa mifumoikolojia ya majini, mabadiliko ya tabia nchi, kuenea kwa viumbe vamizi wageni, kuongezeka uzalishaji wa taka hatarishi ikiwemo taka za kieletroniki. Shughuli zinazochangia uharibifu huo ni pamoja na:- kilimo kisicho endelevu katika maeneo ya vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kwenye vilele vya milima, miteremko ya safu za milima na uendeshaji wa shughuli za kilimo cha umwagiliaji usioendelevu; ufugaji wa kuhama hama na unaopelekea makundi makubwa ya mifugo kutafuta malisho na maji; ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa pamoja na upanuzi wa mashamba na makazi, matukio ya mara kwa mara ya uchomaji moto wa misitu; na uchimbaji wa madini usio endelevu. Aidha, upo uhusiano mkubwa kati ya umaskini na uharibifu wa mazingira kwani asilimia kubwa ya wananchi hutegemea matumizi ya maliasili inayowazunguka katika kuendesha maisha yao ya kila siku hali ambayo husababisha utumiaji wa maliasili usioendelevu na kuleta uharibifu wa mazingira. Ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira, serikali imeandaa sera, sheria na miongozo mbalimbali ya hifadhi ya mazingira. Aidha, katika miaka ya hivi karibuni pamekuwepo na juhudi za uhamasishaji wa wananchi katika masuala ya hifadhi ya mazingira na hivyo kuleta ongezeko la uelewa kuhusu umuhimu na manufaa ya kuhifadhi mazingira kwa baadhi ya vikundi vya jamii na asasi nyingi nchini. Hata hivyo, ushiriki wa wananchi katika hifadhi ya mazingira bado hauridhishi.

Kwa kutambua hayo, Serikali ilianzisha mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji Kupanda na Kutunza Miti. Madhumuni ya mashindano ni kuchochea na kutia hamasa wananchi kushiriki katika hifadhi ya mazingira kwa lengo la kudhibiti kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na hatimaye kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji nchini.

Ili kuongeza wigo na ushiriki katika mashindano na kuboresha tuzo hiyo, Serikali imefanya marekebisho katika Mwongozo wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti ya mwaka 2008 ili utumike katika mchakato wa uendeshaji wa Mashindano ya Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira. Maboresho haya yamezingatia makundi ya ushindani na

vigezo vya ushindani. Mwongozo huu umezingatia mambo muhimu yafuatayo; madhumuni ya tuzo; vigezo vitakavyotumika; ngazi za ushindani na makundi husika; ushiriki na uhamasishaji; utoaji wa Tuzo  na thamani ya tuzo; uteuzi wa Washindi, utaratibu wa kutoa na kukabidhi tuzo; gharama; majikumu ya wadau na ratiba ya utekelezaji. Tuzo hii itatolewa kila baada ya miaka miwili kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Ni matumaini yangu kuwa Mwongozo huu utaboresha uendeshaji wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira pia utaongeza wigo wa ushiriki wa wananchi na hatimaye kuchangia katika juhudi za hifadhi ya mazingira ya nchi yetu.

January Y. Makamba (MB)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**MUUNGANO NA MAZINGIRA**

# SHUKRANI

Kukamilika kwa Mwongozo huu wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ni matokeo ya Jitihada za dhati za wadau mbalimbali wa sekta ya mazingira hapa nchini.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote kwa michango yao iliyowezesha kukamilisha Mwongozo huu. Ni vigumu kuwataja wote walioshiriki kwa majina, Hata hivyo, kwa namna ya pekee nawashukuru wafuatao kwa kuwa mstari wa mbele katika kutafuta rasilimali, kusimamia uandishi na kushiriki katika kuboresha mwongozo huu. Wadau walioshiriki katika warsha za kikanda zilizoendeshwa nchini; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikli za Mitaa (TAMISEMI); Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mhandisi Joseph Kizito Malongo
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# YALIYOMO


**DIBAJI** ..... i

**SHUKRANI** ..... iii

**1. UTANGULIZI** ..... 1

**2. MADHUMUNI YA TUZO** ..... 1

**3. VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KUTATHMINI** ..... 2

**4. NGAZI ZA USHINDANI NA MAKUNDI HUSIKA** ..... 3
- 4.1 Ngazi za Ushindani ..... 3
- 4.2 Makundi ya Ushindani ..... 3

**5. WASHINDI WA KITAIFA** ..... 4

**6. USHIRIKI NA UHAMASISHAJI** ..... 4

**7. UTOAJI WA TUZO NA THAMANI YAKE** ..... 4

**8. UTEUZI WA WASHINDI** ..... 5
- 8.1 Ngazi ya Mkoa ..... 5
- 8.2 Ngazi ya Kitaifa ..... 5

**9. KAMATI ZA KUTEUA WASHINDI** ..... 5
- 9.1 Kamati ya uteuzi ..... 5
- 9.2 Jopo la wataalam ..... 5

**10. MCHAKATO WA KUPATA WASHINDI WA KITAIFA** ..... 6

**11. KUPATA WASHINDI WA KATA, WILAYA NA MKOA** ..... 7

**12. UTARATIBU WA KUTOA NA KUKABIDHI TUZO** ..... 8

**13. GHARAMA** ..... 8
- 13.1 Halmashauri/Miji/Manispaa ..... 9
- 13.2 TAMISEMI ..... 9
- 13.3 Ofisi ya Makamu wa Rais ..... 9

**14. AINA YA TUZO NA THAMANI YAKE** ..... 10

**15. RATIBA YA UTEKELEZAJI** ..... 10

**16. FOMU YA KUJIANDIKISHA** ..... 11

**17. FOMU YA KUTATHMINI MSHIRIKI WA TUZO** ..... 11

# 1. UTANGULIZI

Tanzania imebahatika kuwa na eneo kubwa lenye rasilimali mbalimbali za kimazingira kama vile bahari, maziwa na ardhi. Pamoja na rasilimali hizi, inakabiliwa na changamoto za uharibifu mkubwa wa mazingira, ukiwemo, uharibifu wa ardhi, kupotea kwa bioanuai na makazi ya wanyamapori, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa mifumoikolojia ya majini, mabadiliko ya tabia nchi, kuenea kwa viumbe vamizi wageni na kuongezeka na kusambaa kwa taka za kieletroniki. Uharibifu huu unatokana na shughuli zisizoendelevu kama vile; kilimo kwenye maeneo ya vyazo vya maji; vilele na miteremko ya safu za milima; ukataji wa miti holela kwa ajili ya kuni na mkaa; uchomaji ovyo wa misitu; uchimbaji wa madini usiozingatia hifadhi ya mazingira; ufugaji wa kuhamahama ili kutafuta malisho na maji; wingi wa mifugo unaozidi uwezo wa malisho; uingizaji na utupaji holela wa taka na vifaa vya kielektroniki. Uharibifu huu umekuwa changamoto kubwa katika hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

# 2. MADHUMUNI YA TUZO

Madhumuni makuu ya Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ni kuongeza kiwango cha ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi mazingira ili kulinusuru taifa letu na majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira. Kupitia Tuzo hii, wananchi watahamasika kushiriki katika shughuli za kuhifadhi mazingira katika maeneo yao kwa lengo la kuboresha hali ya mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Madhumuni mahsusi ya Tuzo ni:-

a) Kutambua juhudi na mchango wa wananchi au vikundi vinavyojishughulisha na hifadhi ya mazingira;
b) Kuhamasisha wananchi ili watambue umuhimu wa kutunza, kusimamia na kuhifadhi mazingira.
c) Kutoa changamoto kwa wananchi ili wawe mstari wa mbele katika kutunza, kusimamia na kuhifadhi mazingira;

d) Kuongeza uwajibikaji kwa watendaji na wadau mbalimbali katika suala la usimamizi wa mazingira; na
e) Kupanua wigo wa ushirikishwaji wa jamii na kuipa jamii madaraka zaidi katika kusimamia kuhifadhi na kutunza mazingira.

## 3. VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KUTATHMINI

Washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira watapatikana kutokana na juhudi za kuhifadhi mazingira katika maeneo yafuatayo:

i) Hifadhi ya vyanzo vya maji na matumizi ya maji;
ii) Upandaji miti;
iii) Uzalishaji endelevu viwandani;
iv) Matumizi ya nishati mbadala;
v) Uchimbaji madini endelevu;
vi) Kilimo endelevu na usimamizi wa taka; na
vii) Ufugaji endelevu na Afya na Usafi wa Mazingira.

Vigezo vitakavyotumika kuwapata washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ni kama ifuatavyo;-

i) **Matumizi ya teknolojia sahihi na endelevu** katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, uzalishaji endelevu viwandani, matumizi ya nishati mbadala, uchimbaji wa madini, kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira.

ii) **Ubunifu katika matumizi ya mbinu za asili za kuhifadhi mazingira** katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, Uzalishaji endelevu viwandani, Matumizi ya nishati mbadala, Uchimbaji wa madini, Kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira

iii) **Utafiti wenye matokeo chanya** katika masuala ya kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, Uzalishaji endelevu viwandani, Matumizi ya nishati mbadala Uchimbaji wa madini, Kilimo,

usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na  ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira

iv) **Ujasiriamali/mbinu za uzalishaji rasilimali** katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, uzalishaji endelevu viwandani, Matumizi ya nishati mbadala, Uchimbaji wa madini, Kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na  ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira

v) **Elimu ya mazingira/utekelezaji wa Sheria za Mazingira**;- Utoaji wa elimu ya Mazingira, uelewa wa sheria ya mazingira zinazohusu shughuli za mshiriki, utekelezaji wa sheria ya mazingira na uwepo wa sheria ndogo za mazingira na utekelezaji wake katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, matumizi ya nishati, uchimbaji wa madini, kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati, ufugaji, utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira.

vi) **Uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake** katika shughuli za uzalishaji viwandani na migodini.

Aidha, vigezo hivi vimefafanuliwa kwenye fomu ya kutathmini mshiriki wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira iliyoko ukurasa 9.

# 4. NGAZI ZA USHINDANI NA MAKUNDI HUSIKA

## 4.1 Ngazi za Ushindani

Mchakato wa kupata washindi wa Tuzo utafanyika katika ngazi za Kata, halmashauri za Wilaya, Manispaa na majiji na hatimaye Mkoa na Taifa.

## 4.2 Makundi ya Ushindani

Mashindano yatahusisha watu binafsi, vikundi vya kijamii, mashirika ya umma, makampuni ya umma na binafsi, wasanifu majengo, wakadiriaji majenzi na wajenzi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), taasisi za umma, shule, vyuo/taasisi za utafiti, majeshi na halmashauri za Wilaya/Mikoa.

## 5. WASHINDI WA KITAIFA

Washindi waliopendekezwa kufikia ngazi ya Taifa watashindanishwa ili kupata mshindi wa kwanda hadi wa tano. Mshindi wa kwanza atachaguliwa kutokana na ubunifu wake wa ziada katika kuhifadhi mazingira kwa ujumla.

## 6. USHIRIKI NA UHAMASISHAJI

Utaratibu wa ushiriki na uhamasishaji katika mashindano ya Tuzo utakuwa kama ifuatavyo:-

i) Wananchi wote katika ngazi mbalimbali watahamasishwa ili kushiriki kwenye mashindano haya. Aidha, Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi na vyombo vya habari vitahusika katika kuhamasisha wananchi ili washiriki katika mashindano haya.

ii) Mshiriki atatakiwa kujiandikisha kuingia katika shindano kwa kujaza fomu za ushiriki zinazopatikana katika ofisi ya Afisa Mtendaji wa Mtaa/ Kijiji, Kata, ofisi za Halmashauri ya Wilaya/Manispaa/ Jiji nchini na baada ya kujaza fomu husika mshiriki atatakiwa kuirudisha katika Ofisi ya mtaa au kijiji katika eneo lake mahali ambapo mchakato wa kupata washiriki utaanzia

## 7. UTOAJI WA TUZO NA THAMANI YAKE

Tuzo zitatolewa kwa washindi katika ngazi ya Kata, Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji na hatimaye Mkoa na Taifa ili kutambua juhudi zao katika kuhifadhi mazingira. Washindi katika Ngazi ya Halmashauri, Wilaya, na Mkoa watapewa Tuzo na halmashauri na Mkoa husika kadri watakavyopanga. Washindi wa katika ngazi ya Taifa watapewa Tuzo na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, thamani za tuzo zinaweza kutofautiana kulingana na bajeti iliyotengwa na serikali katika ngazi za Halmashauri, Mikoa na Wizara. Kwa muktadha huo, thamani ya tuzo inaweza kubadilika mwaka hadi mwaka. Thamani za tuzo kwa washindi wa kitaifa zimeoneshwa kwenye kiambatisho namba 1.

# 8. UTEUZI WA WASHINDI

## 8.1 Ngazi ya Mkoa

Uteuzi wa washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira utaanzia kwenye mikoa husika katika ngazi za kijiji/mtaa, kata, wilaya, mikoa na hatimaye kupata washindi wa kitaifa kwa kila kundi la ushindani.

## 8.2 Ngazi ya Kitaifa

Katika ngazi hii kutakuwa na **Kamati ya Uteuzi** na **Jopo la Wataalam**. Uteuzi wa mshindi utafanywa baada ya Kamati ya uteuzi kupitia mapendekezo ya Jopo la Wataalamu. Kamati itateua washindi wa kitaifa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kwa hatua mstahiki.

# 9. KAMATI ZA KUTEUA WASHINDI

## 9.1 Kamati ya Uteuzi

Kamati ya uteuzi itakuwa na wajumbe watano (5) ambao watateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Kwakuwa Tuzo hiyo hutolewa kila baada ya miaka miwili (2) uteuzi wa wajumbe hao utadumu kwa muda wa miaka sita (6).

## 9.2 Jopo la Wataalam

Ofisi ya Makamu wa Rais itaratibu uteuzi wa Wajumbe wa Jopo la wataalam ambao watakuwa wameteuliwa na Wizara/Taasisi husika. Jopo litaundwa na maafisa waandamizi na litatathmini mapendekezo ya Kamati za Uteuzi za mikoa na kufanya ukaguzi wa maeneo ya washindi waliopendekezwa kwa kufuata vigezo vilivyowekwa. Aidha, jopo litatoa mapendekezo ya washindi kwa

**Kamati ya Uteuzi ya kitaifa**. Jopo litaundwa na wajumbe toka sekta na taasisi zifuatazo:-

i) Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa);
ii) Ofisi ya Makamu wa Rais;
iii) Wizara ya Maliasili na Utalii;
iv) Wizara ya Maji na Umwagiliaji;
v) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
vi) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
vii) Wizara ya Kilimo;
viii) Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
ix) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
x) Wizara ya Nishati;
xi) Wizara ya Madini; na
xii) Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

## 10. MCHAKATO WA KUPATA WASHINDI WA KITAIFA

i) Mchakato utaanza ngazi ya Kata.

ii) Mapendekezo ya washindi wa kila kundi walliotokana na michuano kwenye ngazi ya kata, wilaya hadi mkoa yatawasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais.

iii) Mapendekezo ya washindi hao yataambatana na maelezo ya aina, kiasi na ukubwa wa shughuli wanazofanya kwa kufuatana na vigezo vilivyowekwa.

iv) Jopo la wataalamu wa kitaifa litafanya uchambuzi wa mapendekezo ya washindi kutoka kila mkoa ili kupata mapendekezo ya washindi ambao watafanyiwa tathmini.

v) Jopo litafanya tathmini na uhakiki kwa kutembelea maeneo ya washindani walioteuliwa ili kupata washindani watakaowasilishwa kwa Kamati ya Uteuzi ya Kitaifa.

vi) Kamati ya Uteuzi itapokea na kufanya uchambuzi wa washindi waliopendekezwa wa nchi nzima na ndio hao watakaotangazwa na kupewa Tuzo na Mheshimiwa Rais.

vii) Kati ya washindi waliopatikana mshindi aliyefanya vizuri zaidi kwa kuonyesha ubunifu wa ziada katika kuhifadhi mazingira ndiye atakayekuwa mshindi wa jumla.

Aidha, mchakato wa kupata washindi wa kitaifa utafanyika kama ifuatavyo;-

**a) Kamati ya uteuzi Ngazi ya Kata**

Katika ngazi ya kijiji/mtaa, kamati ya mazingira ya kijiji/mtaa itatathmini na kupendekeza washindani watakaojiandikisha kwa kamati ya mazingira ya kata. Katika ngazi ya kata kamati ya mazingira ya kata itatathmini na kupendekeza washindani kwa jopo la wataalam wa halmashauri za wilaya.

**b) Kamati ya Uteuzi Ngazi ya Wilaya na Mkoa**

Katika ngazi za mikoa na wilaya, makatibu tawala mkoa na wilaya wataratibu zoezi hili kwa kushirikiana na wakurugenzi wa halmashauri. Aidha, watateua kamati za uteuzi zenye wajumbe watano (5) na jopo la wataalam katika mikoa na halmashauri zao. Jopo la wataalam kimkoa na halmashauri za wilaya litateuliwa kwa kufuata mfumo wa jopo la kitaifa.

## 11. KUPATA WASHINDI WA KATA, WILAYA NA MKOA

i) Mchakato utaanzia ngazi ya kata kwa kushindanisha makundi yaliyopo kwenye ngazi ya vijiji / mtaa.Kata zitateua washindi wa kata kati ya mapendekezo waliyopokea na kupeleka ngazi ya wilaya kwenye jopo la wataalamu na kamati ya uteuzi, kwa uchambuzi.

ii) Halmashauri za Wilaya zitapokea na kutathmini washindani toka katika kata zake zote ili kupata washindi wa wilaya watakaopelekwa katika ngazi ya mkoa.

iii) Kila mkoa utateua washindi wa mkoa na kuwasilisha Ofisi ya Makamu wa Rais mapendekezo ya washindi walioteuliwa ili kuingia katika mchakato wa kupata mshindi wa Kitaifa.

## 12. UTARATIBU WA KUTOA NA KUKABIDHI TUZO

Utoaji wa Tuzo utafanyika kila baada ya miaka miwili katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni.

Ofisi ya Makamu wa Rais itasimamia na kuratibu utoaji wa Tuzo katika ngazi ya taifa. Aidha, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itaratibu uendeshaji wa Tuzo katika ngazi za mikoa ambapo mpango wa utekelezaji na taarifa ya mchakato wa kupata washindi utawasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa wakati husika. Vilevile, halmashauri za wilaya zitasimamia katika ngazi za wilaya, kata, na vijiji/mtaa. Tuzo itatolewa iwapo vigezo vilivyoandaliwa vitafikiwa kwa kiwango kitakachoridhisha Jopo.

Tuzo za washindi wa kitaifa zitatolewa na Mheshimiwa Rais na vyeti vya washindi wote wa kitaifa vitasainiwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe. **Aidha, katika ngazi ya Mkoa na Wilaya utaratibu uwekwe na mamlaka husika ili washindi katika ngazi hizo wapewe zawadi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.** Majina ya washindi wa kitaifa wa Tuzo ya Rais ya kuhifadhi Mazingira yatangazwe katika wilaya na mikoa yao ili kuleta hamasa katika jamii.

## 13. GHARAMA

Fedha za kugharamia mchakato na utoaji wa Tuzo zitatoka katika bajeti ya serikali. Vilevile, wadau wengine yakiwemo mashirika binafsi, makampuni, taasisi na watu binafsi wanahamasishwa kuchangia gharama za mchakato na

utoaji wa Tuzo hii. Aidha, bajeti za Halmashauri/Miji/Manispaa husika, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Makamu wa Rais zitatumika kama ifuatavyo:-

### 13.1 Halmashauri/Miji/Manispaa

Halmashauri zitagharamia mchakato wa uhamasishaji, kupata washindi na kukabidhi Tuzo katika ngazi za wilaya, Kata na vijiji. Hii ni pamoja na gharama za usafiri, posho na malazi kwa kamati za uteuzi, jopo la wataalam na washindi.

### 13.2 TAMISEMI

Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itagharamia mchakato wa uhamasishaji, kupata washindi na kukabidhi Tuzo katika ngazi ya mkoa. Aidha, Kila halmashauri itaumia radio zake kuhamasisha wananchi kuingia kwenye mashindano hayo. Wananchi watahamasishwa pia wakati wa maadhimisho ya kitaifa na sherehe za ki-wilaya na halmashauri kwa kutumia hotuba za viongozi, na vikundi vya sanaa. Pia viongozi wa dini waombwe kuhamasisha waumini wao kujiandikisha kushiriki mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira. Kila mkoa utagharamia usafiri, posho na malazi kwa kamati za uteuzi, jopo la wataalam na washindi.

### 13.3 Ofisi ya Makamu wa Rais

Ofisi ya Makamu wa Rais itagharamia kamati ya uteuzi, jopo la wataalam na washindi wa ngazi ya Taifa. Hii ni pamoja na gharama za usafiri, posho na malazi. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itagharamia zawadi za vyeti, fedha taslimu, Kombe na ngao kwa washindi wa ngazi ya kitaifa.

## 14. AINA YA TUZO NA THAMANI YAKE

| WASHINDI KITAIFA | TUZO<br>ZAWADI NYINGINE | |
|---|---|---|
| | FEDHA TASLIMU | ZAWADI NYINGINE |
| Mshindi wa Kwanza | 5,000,000.00 | Pikipiki na Cheti |
| Mshindi wa Pili | 4 ,000,000.00 | Pikipiki na Cheti |
| Mshindi wa Tatu | 3,000,000.00 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Nne | 1,500,000.00 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Tano | 1,000,000.00 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Jumla | 2,000,000 | Ngao |

## 15. RATIBA YA UTEKELEZAJI

| SHUGHULI/TUKIO | **MUDA** (kila baada ya miaka miwili) | MHUSIKA |
|---|---|---|
| Kuanza mchakato wa kupata washindani (kutoa matangazo, kuhamasisha, kuandikisha, tathmini) | Julai | Wizara zote,OMR TAMISEMI, Halmashauri/Miji/Manispaa, AZISE |
| Kupata mshindi ngazi ya kijiji na kuwasilisha Kata | Desemba | Halmashauri/Miji/Manispaa |
| Kupata mshindi ngazi ya Kata na kuwasilisha Wilayani | Januari | Halmashauri/Miji/Manispaa |
| Kupata mshindi ngazi ya wilaya na kuwasilisha mkoani | Februari | Halmashauri/Miji/Manispaa |
| Kupata washindi ngazi ya mkoa na kuwasilisha OMR | Machi | TAMISEMI |
| Kutembelea maeneo na kufanya ukaguzi ili kuhakiki | Aprili | OMR |
| Kupata washindi ngazi ya taifa | Mei | OMR |
| Kutoa Tuzo | Tarahe 5 Juni | OMR, TAMISEMI<br>Halmashauri/Miji/Manispaa |

## 16. FOMU YA KUJIANDIKISHA

**FOMU YA KUJIANDIKISHA KUSHIRIKI MASHINDANO YA TUZO YA RAIS YA KUHIFADHI MAZINGIRA**

**SEHEMU A: MAELEZO BINAFSI**

Jina la mshiriki…………………………………………….……………………

Jinsia…………………………………………………………………………

Anuani ya Mshiriki:

Kijiji/Mtaa………………………………………………......….. Kata.....................................................................

Wilaya/Miji/Manispaa.........................................................Mkoa..................................

Sandukula Posta........................................

Namba ya simu.......................................................

Barua Pepe.................................................................

**SEHEMU B: MAELEZO MAFUPI YA SHUGHULI ANAZOFANYA KATIKA KUHIFADHI MAZINGIRA**

.......................................................................................................................................................

.......................................................................................................................................................

.......................................................................................................................................................

.......................................................................................................................................................

SAINI YA MSHIRIKI…………………………………………. SAINI YA MTENDAJI KIJIJI/MTAA/KATA/WILAYA/MKOA

TAREHE…………………………………………………. TAREHE……………………………………………………

***ANGALIZO:*** *BAADA YA FOMU KUJAZWA, ZIWASILISHWE KWA WATENDAJI KATIKA MAENEO HUSIKA KWA AJILI YA KUWASILISHWA KWENYE HALMASHAURI*

TUNAKUSHUKURU KWA KUAMUA KUSHIRIKI KWENYE MASHINDANO YA TUZO YA RAIS YA KUHIFADHI MAZINGIRA

---

## 17. FOMU YA KUTATHMINI MSHIRIKI WA TUZO

**FOMU YA TATHMINI**

Jina la Mshindani.........................................................................................................

Jinsia............................................................................................................................

Kijiji.....................................................Kata..................................................................

Tarafa..................................Wilaya.............................. Mkoa...................................

Anuani............................................................................................................................

Namba ya simu............................................Barua Pepe…………………………………..

Saini na Muhuri...............................................Tarehe...................................................

| | Vigezo | Kiwango* | Maoni |
|---|---|---|---|
| 1 | **Matumizi ya tekonolojia katika hifadhi ya mazingira** | | |
| | **UHIFADHI WA MAJI NA VYANZO VYA MAJI** | | |
| | Jinsi anavyohifadhi vyanzo maji | | |
| | Jinsi anavyohifadhi maji | | |
| | Njia anayotumia kujipatia maji kwa matumizi yake | | |
| | Jinsi anavyotumia maji | | |
| | **USIMAMIZI WA TAKA NA MAJITAKA** | | |
| | Jinsi anavyokusanya na kutupa maji taka | | |
| | Anavyodhibiti taka ngumu na kurejeleza | | |
| | Anavyotunza na kusimamia taka hatarishi (vyuma chakavu, plastiki, mafuta machafu, taka za kielektroniki, betri zilizotumika n.k) | | |
| | Matumizi na aina ya choo anachotumia | | |
| | Utunzaji wa Mazingira ya Choo | | |
| | **MATUMIZI YA NISHATI MBADALA** | | |
| | Aina ya Nishati anayotumia | | |
| | Njia ya matumizi ya nishati na Uhamasishaji | | |
| | **UCHIMBAJI MADINI** | | |
| | Aina ya teknolojia | | |
| | Matumizi endelevu ya teknolojia | | |
| | Uchimbaji wa madini unaozingatia hifadhi ya Mazingira | | |
| | **SHUGHULI ZA KILIMO ENDELEVU** | | |
| | Aina ya kilimo anacholima | | |
| | Aina ya pembejeo anazotumia | | |
| | Aina ya mbolea anayotumia | | |
| | Matumizi sahihi ya maji katika kumwagilia mashamba | | |
| | **SHUGHULI ZA UFUGAJI ENDELEVU** | | |
| | Aina ya ufugaji anaotumia | | |
| | Matumizi ya mazao ya mifugo(Kinyesi, ngozi, maziwa, nyama nk) | | |
| 2 | **Utafiti kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mazingira** | | |
| | **MAJI** | | |
| | Idadi ya vyanzo maji | | |
| | Changamoto za hifadhi ya vyanzo vya maji | | |
| | Mbinu za kutatua changamto za uharibifu wa vyanzo vya maji | | |
| | Takwimu za matumizi ya maji | | |
| | **TAKA** | | |
| | Udhibiti na usimamizi wa maji taka | | |
| | Mbinu endelevu za Usimamizi wa taka ngumu | | |
| | Changamoto Usimamizi wa taka za kiielektroniki | | |
| | Mbinu endelevu za usimamizi wa taka ngumu | | |
| | **NISHATI** | | |
| | Matumizi ya nishati mbadala na majiko banifu | | |
| | Changamoto za matumizi ya Nishati ya kuni na mkaa | | |
| | **UCHIMBAJI WA MADINI** | | |
| | Aina ya Teknolojia | | |
| | Matumizi ya teknolojia endelevu | | |
| | Athari kwa Mazingira | | |
| | **KILIMO** | | |
| | Mbinu bora za kilimo | | |
| | Matumizi ya kilimo hifadhi | | |
| | **UFUGAJI** | | |
| | Mbinu za ufugaji bora | | |
| | | | |
| 3 | **Matumizi ya mbinu za asili katika hifadhi ya mazingira** | | |
| | **MAJI** | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kuhifadhi uhifadhi  vyanzo maji | | |
| | Kuhifadhi  maji | | |
| | Upatikanaji wa maji | | |
| | Matumizi ya maji | | |
| | **TAKA** | | |
| | Usimamizi wa maji taka | | |
| | Usimamizi wa taka ngumu | | |
| | Usimamizi wa taka za kiielektroniki | | |
| | **KILIMO** | | |
| | Aina ya mbolea | | |
| | Aina ya kilimo | | |
| | Aina ya pembejeo | | |
| | **NISHATI** | | |
| | Elimu kuhusu mbinu za asili za  Matumizi bora ya Nishati | | |
| | Mbinu za matumizi bora ya nishati | | |
| | **UFUGAJI** | | |
| | Ufahamu kuhusu mbinu bora za kiasili za ufugaji | | |
| | Matumizi ya mbinu bora za kiasili za ufugaji | | |
| | | | |
| 4 | **Upandaji miti na shughuli za uoto wa asili** | | |
| | Kuwepo kwa shamba la miti | | |
| | Kuwepo kwa vitalu vya miti na kusambaza kwa jamii | | |
| | Idadi ya miti iliyopandwa | | |
| | Hali ya usitawi wa miti iliyopandwa | | |
| | Aina ya miti iliyopandwa | | |
| 5 | **Ujasiliamali/mbinu za uzalishaji rasilimali zinaozingatia hifadhi ya mazingira** | | |
| | Matumizi ya taka kama njia ya kuongeza kipato | | |
| | Urejelezaji wa taka | | |
| | Upandaji miti | | |
| | Matumizi ya maliasili kama njia ya kujiongezea kipato | | |
| **6** | Elimu ya Mazingira na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira | | |
| | | | |
| | Utoaji wa elimu ya Mazingira | | |
| | Uelewa wa  sheria ya mazingira zinazohusu shughuli za Mshiriki | | |
| | Utekelezaji wa sheria ya Mazingira | | |
| | Uwepo wa sheria ndogo za mazingira na utekelezaji wake | | |

**Kiwango*: 0 = Hakuna; 1 = Dhaifu; 2 = Wastani; 3 = Nzuri; 4 = Nzuri sana; H= Haihusiki**

Jina la Mhakiki ngazi ya kijiji/mtaa/kata/wilaya/mkoa/taifa.......................................................

Saini.....................................................................Tarehe.....................................................